# Yesu Mwokozi Wetu – Kristo Bwana

**na**

**Terry Warford**

# Yesu Mwokozi Wetu – Kristo Bwana

**na**

**Terry Warford**

**Novemba 5, 2011**

# Yesu Mwokozi Wetu – Kristo Bwana

Katika sura ya pili ya Luka, malaika aliwatokea wachungaji kuwaambia kuhusu Yesu. Luka 2:10-11, "*Malaika akawaambia, msiogope kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote; maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa kwa ajili yenu, Mwokozi ndiye Kristo Bwana.*"

Watu wengi wamesikia kuhusu Yesu, na wanaweza kufahamu kidogo kumhusu. Tunachotarajia kukamilisha katika makala haya ni kutoa hitoria ya Yesu iliyowekwa katika mazingira ya kihistoria. Tunatarajia kusema historia yake kwa njia ambayo ni rahisi kwa mtu mpya katika injili kuweza kufuatilia. Tunatarajia kueleza ni kwa nini Yesu alikuja katika ulimwengu huu, alichokuja kukamilisha, na jinsi alivyofanya, ili kwamba tuweze kuona alichomanisha kwetu.

Ni agenda kubwa, na tunaomba kwamba itafundisha.

Awali ya yote, historia ya Yesu haianzi na kuzaliwa kwake katika ulimwengu huu. Historia ya Yesu kwa hakika inaanzia katika uumbaji wa ulimwengu. Ukisoma sura ya kwanza ya Mwanzo, utaona kwamba Mungu akasema huu ulimwengu ukawepo, na akanena katika uwepo wa vitu vyote kuujaza. Zab. 33:8-9 inatupatia mukhutasari wa hili, "*Nchi yote na imwogope BWANA, wote wakaao duniani na wamche. Maana yeye alisema, ikawa; nay eye aliamuru, ikasimama.*" Mustari wa 6 unasema, "*Kwa neno la BWANA mbingu zilifanyika, na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake.*"

Yesu ni neno la Mungu, ambayo ndiyo aliyoumbia dunia, kama tunavyosoma katika Yoh. 1" 1-3, "*Hapo mwanzo kulikuwako neno, naye neno alikuwako kwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika.*" Mustari wa 14 unatuambia kuwa neno hili lilikuwa Mwana wa Mungu, "*Naye neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli.*" Mustari wa 17 unamtambulisha Mwana wa Mungu – amejaa neema na kweli – kama Yesu, "*Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa, neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo.*"

Mwanadamu alikuwa ni moja kati ya vitu ambavyo Mungu aliumba kupitia Neno lake, Jesu. Mwa. 1:26-27, "*Mungu akasema na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu wakatawale samaki wa baharini na ndege wa angani, na wanyama na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa*

*kitambaacho juu ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimumba mwanamume na mwanamke aliwaumba.*"

Mungu alimwumba mwanadamu kwa agizo moja tu, lakini agizo hili mwanadamu alilivunja. Dhambi moja hii, iliruhusu dhambi kuingia mlangoni, na kuleta kifo katika ulimwengu huu. Tangia hapo wote wamefanya dhambi, na kufa kwa sababu ya dhambi zao. Inahuzunisha, lakini ni kweli, hadithi inasimuliwa katika sura ya 2 na 3 ya kitabu cha Mwanzo, lakini imetolewa mukhtasari katika Rum. 5:12, "*Kwa hiyo kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi.*"

Maandiko ya Agano la Kale yanaendeleza historia ya Mungu na mwanadamu. Yameegemea sana katika uzao wa Ibrahimu kupitia Isaka na Yakobo. Fil. 2:5-7 inatuambia kwamba hata wakati wa kipindi hicho kabla ya kuzaliwa kwake Yesu alikuwa akitenda kazi na sawa na Mungu lakini alichagua kumtumikia. "*Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu, ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namma ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sana na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya utumwa, akawa ana mfano wa mwanadamu.*". 1 Kor. 10:4 inatupa mfano mmoja ya mambo ambayo Yesu alifanya katika kumhudumia Mungu. Inazungumzia wakati uzao wa Ibrahimu ulipokuwa katika jangwa wakitoka utumwani Misri. "*Wote wakanywa kinywaji kile kile cha roho; kwa maana waliunywea mwamba war oho uliowafuata; na kwamba ule ulikuwa ni Kristo.*"

Wakati wa Agano la Kale, na kuendelea leo, mwanadamu bado anahangaika na dhambi. Wanaume na wanawake wazuri bado wanajikwaa, na ndivyo ilivyo hata kwetu. Dhabihu zilianzishwa na Mungu na kutolewa na mwanadamu, lakini tu ilikuwa ni kwa muda uliowekwa. Ebr. 10:4, "*Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi.*"

Hii inatuongoza tena kwa Yesu. Sababu ambayo Yesu Kristo Neno la Mungu kuja hapa ulimwenguni ilikuwa ni kuchuku dhambi zetu mara moja kwa yote, kama malaika alivyomwelezea Yusufu katika Mt. 1:21, "*Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.*" Malaika aliyewatokea wachungaji Yesu alipozaliwa malaika wengine waliungana naye, Luka 2:13-14, "*Mara walipokuwapo pamoja na huyo malaika, wingi wa jeshi la Mbinguni, wakimsifu Mungu na kusema, atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowarudhia.*" Hakuja kuhitimisha vita, bali kutulea amani na Mungu kwa kuziondoa dhambi zetu. Ebr. 9:28 (sehemu ya mwisho ya mustari) inasema, "*…Akiisha kutikea mara moja*

*azichukua dhambi za watu wengi; atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu.*"

Nayo ilikuwa dhabihu. Yesu alipata maumivu makali na kifo cha kutisha ili kutusamehe dhambi zetu. Rudi katika Fil. 2, tunasoma katika 7-8, "*Bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa mwanadamu; tena alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.*" 1 Pet. 3:18, "*Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu, mwili wake akauawa, bali roho yake akahuishwa.*"

Fungua Biblia yako, au azima kama hauna. Geukia katika vitabu vya Mathayo, Luka, na Yohana; na usome jinsi Yesu alivyoteseka. Usome jinsi walivyomdhihaki, akachekwa, akatemewa mate, akapigwa makofi, akapigwa na kuchapwa. Soma jinsi alivyopigwa misumari, na akainuliwa juu ya msalaba kwa masaa kabla hajafa. Soma na uelewe, jinsi ambavyo angeweza kukomesha zoezi hilo wakati wo wote. Kama ukirudi katika sura ya 37 katika Agano la Kale, utaona kwamba malaika mmoja alishinda jeshi lote. Yesu angeweza kuliita jeshi la malaika ili kuweza kumwokoa. Kwa sababu hakufanya hivyo, alikuwa anafanya dhabiu kuu, dhabiu bora, akijitoa kwa ajili yetu. Soma jinsi alivyowasahe hata wale waliokuwa wakimpiga. Soma jinsi walivyomchoma, hata baada ya kufa. Elewa kwamba hii ilikuwa ni kwa ajili yako, ili dhambi zako ziweze kusamhewa, ili uweze kuwa na uhusiano na Mungu. Vyote ulipewa kupitia upendo wa Mungu na upendo wa Yesu Kristo.

Uligundua tuliposoma 1 Pet. 3:18 hapo juu, ya kwamba hata ingawa Yesu aliuawa katika mwili, pia aliuishwa na Roho? Kuuishwa inamanisha kufanywa hai, au kufufuliwa katika wafu. Ingawa Yesu alikufa, kaburi ambalo alizikwa isingeweza kuwa Neno la Mungu. 1 Kor. 15:3-4, "*Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko.*" Ukiendelea kusoma hadi mustari wa 9 utakuta kwamba zaidi ya watu 500 walimwona Yesu baada ya kufufuka. Hii siyo hadithi, bali ni historia, ukweli uliothibitishwa. Ilitokea. Ni kweli.

Mmoja kati ya wale waliomwona Yesu baada ya kufufuka kwake ni mtume Yohana. Yesu alimtokea wakati Yohana akiwa uhamishoni katika kisiwa cha Patimo. Yesu akamwambia Yohana katika Ufu. 1:18, "*Na aliye hai; nami nalikuwa nimekufa, na tazama, na tazama ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu.*" Hii inamanisha kwamba si tu kwamba Yesu alifufuka ktoka katika wafu; bali pia atasababisha sisi kufufuliwa kutoka katika wafu siku kuu ya hukumu. 1 Kor. 15:21-23, "*Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu,*

*kadhalika na kiyama ya watu ililetwa na mtu. Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa. Lakini kila mmoja mahali pake; limbuko ni Kristo; baadaye walio wake Kristo atakapokuja.*"

Maisha yetu kama Wakristo yanamzunguka Kristo.

Hatua ambazo zipo katika mpango wake wa wokovu, (Kusikia neno, Imani, Toba, Kukiri, na Kubatizwa), inafikia kilele katika kutuweka ndani ya kifo cha Kristo, maziko, na kufufuka. Rum. 6:3-4, "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*"

Moja kati ya sababu kuu inayotusababisha kukusanyika siku ya kwanza ya juma ni kumkumbuka Yesu, na jinsi alivyotufia. 1 Kor. 11:23-26, "*Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, naye akiisha kushuru akaumega, akasema huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema kikombe hiki ni angano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo kwa ukumbusho wangu. Maana kila mwulapo na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.*"

Tunapo kumbuka ushujaa wake, upendo, na msamaha, inapaswa kutapa msukumo wa kuishi kila siku kwake, 2 Kor. 5:14-15, "*Maana upendo wa Kristo watudibisha , maana tumehukumu hivi, ya kwamba mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi walikufa wote; tena alikufa kwa ajili ya wote, ili walio hai wasiwe hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye aliyekufa, akafufuka kwa ajili yao.*"

Mungu anatupa baraka nyingi kupitia Yesu Kristo. Hebu tuchukue tahadhari ya mambo mawili kabla hatujafunga makala haya.

Mungu alitupa neno lake kupitia mwanaye Yesu Kristo. Inaweza kuonekana upuuzi tukisema alitupatia Neno kupitia Neno, lakini ni muhimu kuelewa hivyo. Ebr. 1:1-2, "*Mungu ambaye zamani alisema na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi anasema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu.*" Ni muhimu, kwamba tunafuata neno la Kristo, badala ya mwanadamu. Katika Yoh. 12:48-49 Yesu alisema, "*Yeye anikataae mimi asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye; neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho. Kwa sababu mimi siku nena kwa nafsi yangu tu; bali Baba aliyenipeleka, yeye mwenyewe ameniagiza nitakayonena na nitakayo sema.*"

Yesu alilijenga kanisa lake, na yeye tu ndiye kichwa chake. Kol. 1:18-19, inamwongelea Yesu, inasema, "*Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani cha kanisa, naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote. Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae;*" Kwa nini tuwe sehemu ya kanisa ambalo ndilo lake? Rum. 16:16, "*Salimianeni kwa busu takatifu. Makanisa yote ya Kristo yawasalimu.*"

Katika muhtasari, hapo mwanzo Yesu alikuwa na Mungu kama neno lake. Alikuwa sawa na Mungu kupitia historia yote, lakini alichagua kumtumikia. Wanadamu wote wa kila aina tulipotea katika dhambi zetu hadi Yesu alipokuja na kutufia msalabani. Alifufuka katika wafu, na kupitia yeye nasi tutafufuka siku moja pia. Yesu ndiye tazamio la maisha yetu ya Ukristo. Yeye ndiye njia inayotufanya kuwa Wakristo. Tunashiriki kifo chake, maziko na ufufuo tunapo batizwa (baada ya kusikia, imani, toba na kukiri). Tunakumbuka kifo chake katika ushirika wa meza yake katika sehemu ya ibada siku ya kwanza ya juma. Kumkumbuka inaweza kutusukuma kuishi kila siku kwa ajili ya Yesu, kufuata neno ambalo Yesu ametupatia kupitia yeye – tukimfuata Yesu kama sehemu ya kanisa lake. Yesu ni Mwokozi wetu – Yeye aliyetuokoa kutoka kutoka katika dhambi zetu. Yesu ni Bwana wetu – Yeye ambaye tunatakiwa kumfuata na kumtii kila siku ya maisha yetu. Hiki ndicho anachomanisha kwetu.

Hebu tufunge na Ebr. 3:6, ambayo inatutia nguvu kuwa waaminifu kwake siku zote za maisha yetu, "*Bali Kristo kama Mwana juu ya nyumba ya Mungu; ambaye nyumba yake ni sisi, kama tukishikama sana na ujasiri wetu na fahari ya taraja letu mpaka mwisho.*"

Katika upendo wa Kristo,

Ndg. Terry Warford